

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THETHINI NA SABA

28 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – TAREHE 28 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Nishati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

306. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaifanya Halmashauri ya Itigi kuwa Wilaya.

307. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ufaulu wa Wanafunzi katika masomo ya Sayansi na Hisabati unaonekana kushuka kila mwaka. Mathalan, mwaka 2015 asilimia 85 ya Wanafunzi walifeli somo la Hisabati matokeo ya Kidato cha Nne. Aidha, katika masomo mengine ya Kemia, Fizikia na Biolojia ufaulu bado ni duni sana:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuinusuru Halmashauri ya Mji wa Tarime na janga hili la ufaulu duni katika masomo ya Sayansi;

(b) Je, nini mkakati wa Serikali katika kuziwezesha maabara za Shule za Sekondari zilizojengwa kwa nguvu kubwa za Wananchi ndani ya Jimbo la Tarime Mjini kwa kuzipatia Wataalam na vifaa vya maabara ili kuinua ufaulu kwenye masomo ya Sayansi.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

308. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENAN (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kuna utaratibu wowote wa kuajiri Watu wote waliohitimu Vyuho na kukidhi vigezo vya kuajiriwa.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

309. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Katika masuala ya Haki za Binadamu Tanzania ina wajibu wa ndani na nje na kila wajibu unahitaji kuonekana wazi ili kujenga

imani kwamba Haki za Binadamu zinatekelezwa katika viwango vya Kisheria, Kikatiba na Kimataifa:-

- (a) Je, Serikali itatimiza vipi matakwa haya ya ndani na nje;
- (b) Je, ni kiasi gani Serikali imekuwa ikijenga misingi ya usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa Haki za Binadamu ndani ya nchi.

310. MHESHIMIWA JANET ZEBEDAYO MBENE (ILEJE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Serikali iliingia Mikataba ya uwekezaji na wadau mbalimbali kwenye Sekta tofauti ambayo kwa sababu mbalimbali imesitishwa na Serikali:-

- (a) Je, ni Mikataba mingapi imesitishwa na ni sekta zipi zinaongoza;
- (b) Je, Serikali imeingia gharama kiasi gani katika kesi zilizofunguliwa Mahakamani kutokana na kusitishwa kwa Mikataba hiyo;
- (c) Je, Serikali imepata faida au hasara gani kwa kusitisha Mikataba hiyo.

WIZARA YA NISHATI:

**311. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY
(MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Serikali iliahidi kupeleka umeme katika Vijiji vyote vya Jimbo la Mbulu Vijijini kupitia REA III kwa sababu REA II haikufanya vizuri katika Jimbo hilo:-

Je, ni Vijiji vingapi vitafikiwa na umeme wa REA Awamu ya III.

**312. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA
(NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Vijiji vya Sintali, Nkana, Nkomachindo na Katani viko kwenye mpango wa kupata umeme wa REA Awamu ya III lakini mpaka sasa hakuna kazi zinazoendelea:-

Je, ni lini kazi hiyo itaanza.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA
TAIFA:**

**313. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(a) Je, ni Vijana wangapi kutoka Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B wamepata nafasi ya kujiunga na Jeshi kuanzia mwaka 2015;

(b) Je, mgawanyo wa idadi ya Vijana wanaojiunga na Jeshi kwa kila Wilaya nchini upoje.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

314. MHESHIMIWA SAADA MKUYA SALUM (WELEZO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na vitendo vya mauaji ya mara kwa mara kwa upande wa Zanzibar katika siku za hivi karibuni; mauaji hayo yanatokana na aidha kuuwawa kwa wanaoshukiwa kuwa ni wezi au mauaji mengine hayajulikani chanzo chake:-

(a) Je, Serikali imeshafanya tathmini juu ya hali hiyo;

(b) Je, ni washukiwa wangapi kwa kipindi cha karibuni ambao wametiwa hatiani kutokana na vitendo vya mauaji kwa upande wa Zanzibar.

315. MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za ujenzi wa Jengo jipya la kisasa la Askari Polisi wa Makunduchi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA
28 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**